

**MWAKILISHI WA CRM LAND CONSULT (T) LIMITED KATIKA UZINDUZI  
WA MPANGO KABAMBE WA MANISPAA YA MUSOMA TAREHE  
27/04/2017**

Mhe Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Katibu Tawala na Mkurugenzi wa Manispaa

Mkuu wa Wilaya ya Musoma

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Musoma

Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa ya musoma

Watendaji wa Taasisi za Serikali

Wananchi na Wadau wa Maendeleo ya Musoma

Mabibi na Mabwana

CRM Land Consult (T) Limited ni kampuni inayomilikiwa na Watanzania kwa asilimia mia moja, ilianzishwa mwaka 2013. Kazi ya uandaaji Musoma Master Plan ilikuwa ni kazi yetu ya kwanza ya Master Plan.

Tunashukuru na kujivunia kuwa kazi hii tumeimaliza vizuri na kwa wakati na kufikia hatua hii ya wewe Mheshimiwa Waziri kuizindua rasmi.

Huu ni Mpango Kabambe wa kwanza kukamilika na kuzinduliwa katika programu hii ya Kuimarisha Halmashauri za Miji Tanzania.

Mheshimiwa Waziri, kama tulivyosema kuwa kazi ya Musoma ilikuwa ni kazi yetu ya kwanza, na kwa kuwa tumeifanya vizuri na kwa weledi, sisi kama kampuni ya kwanza ya kizalendo tunaamini kuwa imefungua milango ya kazi zingine. Kwa sasa kampuni ya CRM inaandaa Mipango Kabambe kwa Halmashauri za Miji na Manispaa za Kigoma-Ujiji, Songea, Moshi, Njombe na Babati.

Kukamilisha kwa kazi yetu ya uandaaji wa Mpango Kabambe ndio mwanzo wa utekelezaji wake. Hivyo nawasihi wadau wote wa maendeleo wa Manispaa ya

Musoma kuitumia kampuni hii kwenye uandaaji wa Mipango kina, urasimishaji na uendelezaji wa maendeleo ya kati.

Mwisho, napenda kuwashukuru kwa dhati Manispaa ya Musoma na wadau wote kwa ushirikiano mliotupa. Tumekua na mawasiliano mazuri na ya karibu yaliyoweza kukamilisha kazi kwa wakati. Vilevile shukrani ziende kwa wananchi wote na wadau wa maendeleo walioshiriki katika kujibu dodoso na kutoa taarifa zilizohitajika katika kukamilisha kazi hii. Pia tunaishukuru Wizara kwa kutoa ushirikiano na ushauri wa kitaalamu katika kukamilisha kazi hii.